
# Matokeo ya Utafiti wa Viashiria vya VVU/UKIMWI na Malaria Tanzania 2011-12

Utafiti wa Viashiria vya VVU/UKIMWI na Malaria Tanzania (THMIS) ulipima kiwango cha maambukizi ya VVU na kutathmini ufahamu, mitazamo na tabia za watu kuhusu VVU/UKIMWI.

### Mwenendo wa Maambukizi ya VVU Tanzania (Bara na Zanzibar kwa Pamoja)

■ 2007-08 THMIS ■ 2011-12 THMIS

*Asilimia ya wenye maambukizi ya VVU*





Kwa ujumla, 5.1% ya Watanzania wenye miaka 15-49 wana maambukizi ya VVU. Kiwango cha maambukizi miongoni mwa wanawake na wanaume kimepungua kutoka 5.7% katika THMIS 2007-08 hadi 5.1% katika THMIS 2011-12.

### Mwenendo wa Maambukizi ya VVU Tanzania Bara (Haihusishi Zanzibar)

■ 2003-04 THIS ■ 2007-08 THMIS ■ 2011-12 THMIS

*Asilimia ya wenye VVU*





Kwa Tanzania Bara, kiwango cha maambukizi ya VVU miongoni mwa wanawake na wanaume miaka 15-49 kimepungua kutoka 7.0% mwaka 2003-04 THIS hadi 5.3% mwaka 2011-12 THMIS. Kupungua kwa maambukizi kati ya mwaka 2003-04 na 2011-12 ni kwa kiwango kikubwa kitakwimu (7.0% dhidi ya 5.3%). Zaidi ya hayo, maambukizi yameonekana kupungua kwa kiasi kikubwa zaidi miongoni mwa wanaume 6.3% dhidi ya 3.9%).

### VVU kwa Makazi

■ Mijini ■ Vijijini ■ Tanzania kwa ujumla


*Asilimia ya wanawake na wanaume miaka 15-49 wenye VVU*




Kiwango cha maambukizi ya VVU ni kikubwa miongoni mwa wanawake (6.2%) kuliko kwa wanaume (3.8%). Watanzania waishio mijini wana uwezekano mkubwa zaidi wa kuwa na maambukizi ya VVU kuliko wale waishio vijijini (7.2% dhidi ya 4.3%).


### VVU kwa Mikoa

*Asilimia ya wanaume na wanawake miaka 15-49 wenye maambukizi ya VVU*




Kiwango cha maambukizi ya VVU kinatofautiana kutoka kiwango cha chini ambacho ni chini ya 1% Pemba na 1.2% Unguja hadi kiwango cha juu 14.8% Mkoani Njombe.

### Kiwango cha Maambukizi ya VVU kwa Umri





Miongoni mwa wanaume na wanawake, kiwango cha maambukizi kwa ujumla kinapanda sambamba na kuongezeka kwa umri. Wanawake wana kiwango kikubwa cha maambukizi kuliko wanaume wa rika lao.

Miongoni mwa wenzi ambao wote wawili walipimwa VVU, 5% walikuwa ni wale ambao mmojawapo ana maambukizi na mwenzake hana maambukizi.

### VVU kwa Hali ya Ndoa

■ Wanawake 15-49 ■ Wanaume 15-49

*Asilimia ya wenye VVU*





*Takwimu katika parandesi zimetokana na matukio 25-49 tu*

Kiwango cha maambukizi ni kikubwa zaidi miongoni mwa wanawake na wanaume ambao ni wajane na waliotalikiana/waliotengana. Wanawake na wanaume ambao hawajawahi kuwa katika ndoa wana uwezekano mdogo wa kuwa na maambukizi ya VVU.

### Ushauri Nasaha na Upimaji wa VVU

2007-08 THMIS | 2011-12 THMIS

*Asilimia ya waliowahi kupima na kupokea majibu*





Ushauri nasaha na upimaji wa VVU umeongezeka kwa kiasi kikubwa; hivi sasa 62% ya wanawake na 47% ya wanaume miaka 15-49 wamewahi kupima VVU na kupokea majibu yao, ukilinganisha na 37% tu ya wanawake na 27% ya wanaume mwaka 2007-08.

Tohara kwa wanaume ni jambo ambalo linafanyika sana nchini Tanzania, ambapo 72% ya wanaume wenye miaka 15-49 wameripoti kwamba wametahiriwa. Kiwango cha kuenea kwa VVU ni 3.3% miongoni mwa wanaume waliotahiriwa na 5.2% miongoni mwa wanaume ambao hawajatahiriwa.

### VVU Miongoni mwa Vijana

Wasichana | Wavulana

*Asilimia ya wasichana na wavulana miaka 15-24 wenye VVU*




**Umri**

Kwa ujumla, 2.0% ya wasichana na wavulana miaka 15-24 wana maambukizi ya VVU. Kiwango cha maambukizi miongoni mwa wasichana ni kikubwa kuliko kwa wavulana, hususani kwa vijana wa miaka 23-24 ambapo wasichana wana uwezekano mkubwa zaidi ya mara mbili wa kuwa na maambukizi kuliko wavulana. (6.6% dhidi ya 2.8%).

***Mwitikio na mfumo wa utafiti:*** *Taarifa za kiwango cha maambukizi ya VVU zilipatikana kutokana na sampuli za damu zilizotolewa kwa hiyari na wanawake na wanaume walioshiriki katika utafiti wa THMIS 2011-12. Kati ya wanawake na wanaume 20,811 wenye miaka 15-49 walioshiriki katika utafiti, 85% walitoa sampuli ya damu kwa ajili ya kupima VVU.*

Kwa taarifa zaidi kuhusu matokeo ya Utafiti wa Viashiria vya VVU/UKIMWI na Malaria Tanzania 2011-12, tafadhali wasiliana na:


**Nchini Tanzania:**
Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)
P.O Box. 76987, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: 255 22 212 2651; Nukushi: 255 22 212 2427
www.tacaids.go.tz

Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)
PO. Box 796, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: 255 22 212 2722; Nukushi: 255 22 213 0852
www.nbs.go.tz

**Nchini USA:**
ICF International
11785 Beltsville Drive
Calverton, MD 20705 USA
Simu: 301-572-0200; Nukushi: 301-572-0999
www.measuredhs.com
www.statcompiler.com



Utafiti wa Viashiria vya VVU/UKIMWI na Malaria Tanzania 2011-12 (THMIS) ulifanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali- Zanzibar (OCGS-Zanzibar) kuanzia Desemba 16, 2011 hadi Mei 24, 2012. Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Zanzibar (ZAC) zilitoa idhini ya kufanyika kwa utafiti huu. Utafiti huu ulifadhiliwa na Shirika la Misaada ya Maendeleo la Watu wa Marekani (USAID), TACAIDS na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (MoHSW). ICF International ilisaidia kufanyika kwa utafiti huu kupitia mradi wa MEASURE DHS unaofadhiliwa na USAID. Mradi wa MEASURE DHS unatoa msaada wa kiufundi na fedha kwa tafiti za demografia na afya katika nchi mbalimbali duniani.


USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

USAID | CDC | President's Malaria Initiative

TANZANIANS AND AMERICANS IN PARTNERSHIP TO FIGHT HIV/AIDS

# Utafiti wa Viashiria vya VVU/UKIMWI na Malaria Tanzania (THMIS) 2011-12

# Kiwango cha Maambukizi ya VVU